

SERA YA KARO YA WILAYA YA SHULE ZA SALT LAKE CITY na MUHTASARI WA MSAMAHYA WA KARO

KAMA UNAHITAJI MSAADA ILI KUIELEWA ILANI HII, TAFADHALI WASILIANA NA BOB MUENCH kuitia
(801) 578-8378.

Mwongozo huu umeandikwa ili kukusaidia kuperuzi sera na taratibu za Wilaya ya Shule za Salt Lake City kuhusiana na misamaha ya karo ya shule na ustahili wa msamaha.

Maelezo Mafupi

1. Sheria ya Utah inaruhusu kutoza karo kwa darasa la saba hadi la kumi na mbili. Hii inamaanisha kwamba mwanafunzi wako anaweza kutozwa karo kwa ajili ya nyenzo, zana, shughuli na programu za shule.
2. Karo zote zinaweza kupata msamaha.
3. Wanafunzi wote wanaokataliwa maombi ya msamaha wa karo wana haki ya kukata rufaa.

Sera ya Wilaya ya Msamaha wa Karo

Bodi ya Elimu ya Wilaya ya Shule za Salt Lake City imepitisha na imeidhinisha sera ya msamaha wa karo na ratiba ya karo kulingana na sheria ya jimbo. Sera, taratibu, na ratiba ya ada zinapatikana kwenye ukurasa wavuti wa wilaya: <https://www.slcschools.org/board-of-education/board-policies> - nenda chini ya ukurasa na utafute S-10: Karo za Wanafunzi na Misamaha ya Karo.

Mchakato wa Msamaha wa Karo

Kila shule ina msimamizi aliyeleteuliwa wa kusamehe ada ambaye anaweza kukagua na kufanya maamuzi kuhusu maombi ya msamaha wa ada. Tovuti ya shule yako au wafanyakazi wa kuwakaribisha watu wanaweza kukupa maelezo ya mawasiliano ya msimamizi wa msamaha wa ada wa shule yako. Wilaya imedhamiria kuhakikisha kwamba mchakato huu wa kupata msamaha wa karo unafanyika kwa haki, bila upendeleo, na bila kuchelewa. Pia, wilaya inahakikisha kwamba mchakato huu unaepuka unyanyapaa, aibu, uangalifu usiofaa, na mzigo usio na sababu kwa wanafunzi na wazazi. Mchakato huu hautakuwa na viashiria vilivyo dhahiri ambavyo vinaweza kumfanya mtu yeote kuwatambua waombaji wa msamaha wa karo, na hakuna wanafunzi wa wilaya (mbali na mwanafunzi ambaye familia/mzazi wake anatumma maombi) wanaoruhusiwa kusaidia mchakato huu wa maombi. Taarifa kutoka kwa familia/wazazi zitahifadhiwa kwa usiri mkubwa wakati wote wa mchakato huu.

Pia, tafadhali fahamu kwamba mwanafunzi anayepewa msamaha wa karo hatatendewa kwa utofauti na wanafunzi wengine, na hataitwa mtu aliyepewa msamaha wa karo kwa wanafunzi wengine, wafanyakazi, au watu wengine ambao hawahitaji kuijua taarifa hiyo.

Ustahili wa Msamaha wa Karo

Mwanafunzi anastahili msamaha wa karo iwapo:

1. anapata chakula cha bure cha mchana chini ya kanuni za USDA
2. mwanafunzi huyo anapokea SSI
3. familia ya mwanafunzi inapokea TANF
4. mwanafunzi huyo anaishi kwenye kituo cha ulezi, au
5. mwanafunzi huyo yupo chini ya uangalizi wa jimbo

Kadhalika, kama una dharura ya kifedha iliyosababishwa na kupoteza kazi, ugonjwa mkubwa, au upotetu mwingine mkubwa wa kipato nje ya uwezo wako, mtoto wako anaweza kuwa na ustahili wa msamaha wa karo hata kama vigezo vingine vya ustahili havijafikiwa. Hata kama mwanafunzi hajafuzu chini ya viwango hivi, bado shule lazima itoe msamaha wa karo iwapo utozaji wa karo unaweza kumnyima mwanafunzi huyo fursa ya kushiriki kikamilifu au kukamilisha matakwa fulani kwa sababu ya kushindwa kulipa karo.

Hata hivyo, ili kufuzu kwa ajili ya msamaha wa karo, shule lazima ipokee NYARAKA ili kuthbitisha ustahili wa mwanafunzi. Unapaswa kujaza fomu sahihi ya Maombi ya Msamaha wa Karo na kuiwasilisha kwa mkuu wa shule kwa ajili ya mapitio na idhini. Maombi yanapatikana kwenye ofisi kuu ya kila shule na kwenye tovuti ya karo za shule ya Bodi ya Elimu ya Jimbo la Utah kuititia:

<https://www.schools.utah.gov/schoolfees?mid=4340&tid=3>. Mara baada ya kuwasilisha fomu zilizojazwa, takwa lako la karo litasimamishwa mpaka uamuvi wa mwisho utakapotolewa kuhusu ustahili wa mwanafunzi wako kwa misamaha ya karo. Iwapo maombi husika yatakataliwa, shule itakutumia Fomu ya Uamuvi na Rufaa. Fomu hii itakuambia kwa nini maombi husika yamekataliwa na kuelezea jinsi unavyoweza kukataa rufaa ya uamuvi huo. Kama utakata rufaa ya kukataliwa misamaha ya karo, huhitaji kulipa karo hadi pale rufaa hiyo itakapotolewa uamuvi.

Kama mwanafunzi wako ana ustahili wa misamaha ya karo, karo zote zinapaswa kusamehewa, ikiwemo – lakini haikomei kwa – zifuatazo:

Ada za kujiandikisha, vitabu vya darasani, amana za vifaa na vitabu vya darasani, zana za shule, kadi za shughuli, michezo, na makabati ya shule; ada za maabara na duka; ada za ukumbi wa mazoezi na taulo; gharama za sare na vikorokoro; ada za ziara za masomo na mikutano; gharama za ziara za darasa au timu; na gharama za ala za muziki zitumikazo kwenye madarasa au shughuli za shule.

Hakuna kitu kama karo “isiyo na msamaha” au ya “hiari”, lakini mbadala wa misamaha ya karo unaweza kuandaliwa katika baadhi ya matukio, lakini si kwa karo ya vitabu vya darasani. Shule haiwezi kukuomba ufanye malipo ya awamu, IOU, au mipangilio mingine ya malipo yaliyochelewa ikiwa unahitimu msamaha wa ada.

Tozo za pete za darasa, vitabu vya mwaka, picha za shule, makoti yenye herufi, na vitu kama hivyo si karo na hazihitaji msamaha. Pia, kama mwanafunzi wako atapoteza au ataharibu mali ya shule, gharama za urejeshi au marekebisho si karo na hazihitaji msamaha. Wanafunzi wanaweza kuhitajika kulipa karo kwa uandikishaji wa masomo yanayokwenda sambamba au kozi za elimu ya juu. Sehemu ya karo inayohusiana mahsusini na chuo au madaraja au alama za baada ya elimu ya sekondari haipo chini ya msamaha wa karo. Kadhalika, ni wanafunzi walitolipa amana ya vitabu vya darasani au ya vifaa tu ndiyo wanaostahili kurudishiwa amana yao mwishoni mwa mwaka wa shule.

Shule na wafanyakazi wa shule hawawezi kuzuia, kupunguza, au kuongeza madaraja au alama, au kuzuia madaraja, alama, ripoti za matokeo, manukuu, au stashahada ili kushurutisha ulipaji wa karo. Shule inaweza kuzuia rekodi rasmi za mwanafunzi kwa mwanafunzi anayewajibika dhidi ya mali ya shule iliyopotea au iliyoharibiwa; hata hivyo, haiwezi kuzuia rekodi za mwanafunzi zinazoweza kumzuia mwanafunzi huyo asihudhurie shule au kupata nafasi katika shule.

Nyaraka za ustahili wa msamaha wa karo HAZIHITAJIKI kila mwaka lakini zinaweza kuhitajika wakati wowote na shule au mzazi anaweza kuomba mapitio kwa nia njema. Pia, hati HAZITADUMISHWA na shule kwa sababu za faragha. Shule inaweza kuhamisha taarifa za ustahili wa msamaha wa karo kwa shule nyingine ambapo mwanafunzi amefaulu au amehamia.

Ikiwa una maswali, ongea kwanza na msimamizi wa kusamehe ada wa shule yako au mwakilishi wa wilaya ya shule aliyeorodheshwa hapa chini:

Idara ya shule ya Uongozi na Utendaji (801) 578-8350

Kama utapenda nakala ya taratibu kamili za wilaya kuhusiana na karo na misamaha ya karo tafadhali wasiliana na Bob Muench kupitia (801) 578-8378.